Stakabadhi ya Ruhusa

Shirika la utafiti la KEMRI-Wellcome Trust: Fomu ya habari na ruhusa ya mgonjwa (Miaka 13-17)

Kichwa cha utafiti: Kuelewa ueneaji, usimamizi na matokeo ya COVID-19 hapa Kenya

Ni nani anayefanya utafiti huu?

Utafiti huu unafanywa na KEMRI ikishirikiana na wizara ya afya. KEMRI ni shirika la kiserikali linalofanya utafiti wa afya kutafuta njia bora za kukinga na kutibu magonjwa siku za usoni kwa manufaa ya kila mmoja.

Utafiti huu unajaribu kujua nini na kwa nini unaombwa kushiriki?

KEMRI kwa sasa inafanya utafiti kujifunza zaidi kuhusu COVID-19. COVID-19 ni ugonjwa unaosababishwa na virusi vipya vya korona vilivyotambuliwa 2019. Katika utafiti huu, tunalenga kujua idadi ya wakenya ambao wameambukizwa virusi vya COVID-19.

Tunawauliza watoto na watu wazima wanaoishi katika maeneo ambayo mfumo wa kufuatilia idadi na afya ya watu unaendelea, katika kaunti ya Kilifi, Nairobi na Kisumu ili washiriki kwenye utafiti huu kwa kupeana sampuli ya damu. Utafiti huu utahusisha watoto 900 wenye umri wa miaka 14 na chini yake, watu 150 wenye umri kati ya miaka 15-19 na watu wazima 1,350 wenye umri wa miaka 20-64.

Unaweza kuchagua ikiwa unataka kushiriki kwenye utafiti huu

Tumezungumza na mzazi wako kuhusu utafiti huu na anajua kwamba tunazungumza nawe. Kushiriki kote kwenye utafiti ni hiari, na uko huru kuamua ikiwa unataka kushiriki au la. Ukikubali kwa sasa, unaweza kubadilisha mawazo yako na uache kushiriki siku za usoni na hakuna mtu atakayekukasirikia. Hii haitakuathiri wewe/huduma ya afya yako sasa au siku za usoni.

Ukikubali kushiriki kwenye utafiti huu, yafuatayo yatafanyika

- Wewe/mzazi wako atapeana habari kukuhusu, kama vile habari za mawasiliano na pale unapoishi
- Damu kama kijiko kimoja cha chai (mililita 5) itachukuliwa kutoka kwa mkono wakokatika kituo cha afya..

Je kuna usumbufu wowote kwa kushiriki?

Kushuhulikia afya yako na ustawi ni jambo la muhimu kwetu. Hatariya kutoa damu kutoka mkononi ni pamoja na usumbufu, kutoka damu na kuumiangozi pale mahali palipodungwa na kwa nadra sana kupata maambukizi. Tutapunguza hayakwa kutumia wafanyikazi wenye mafunzo ya juu na vifaa safi kwa taratibu zote. Ukipata maambukizi kwenye ngozi, kwa kawaida yataisha haraka.

Utanufaika vipi kwa kushiriki kwenye utafiti huu?

Hakuna manufaa ya moja kwa moja kwako kwa kushiriki. Kuna manufaa kwa jamii nzima kwa kutusaidia kuelewa mifumo ya usambazaji wa COVID-19 hapa Kenya.

Kutafanyika nini kwenye sampuli

Majina ya watu binafsi yataondolewa kwa sampuli zote na badala yake kuwekwe nambari maalum, kuhakikisha sampuli zinaweza tu kuambatanishwa na washiriki na watu wanaohusika na utafiti kwa ukaribu. Baadhi ya vipimo vya utafiti vitakavyofanywa kwenye sampuli vitafanywa kwenye maabara ya KEMRI Kilifi. Sehemu ya sampuli itatumwa kwa maabara ya ng'ambo, katika chuo kikuu cha Rockefeller Marekani, na kitengo cha utafiti cha Mahidol Oxford Tropical Medicine huko Thailand. Baada ya utafiti, sehemu ndogo ya sampuli za damu itahifadhiwa kwenye maabara ya KEMRI Kilifi. Siku za usoni, utafitimpya kuhusu ugonjwa wowote unawezakufanywa kwenye sampuli hizi. Hii inaweza kujumuisha kusafirisha sampuli ng'ambo kwa vipimo vya utafiti. Tafiti za siku zijazo ni lazima kwanza ziidhinishwe kabla zianze na kamati ya wataalam ya kitaifa iliyo huru ili kuhakikisha kwamba usalama na haki za washiriki zinaheshimiwa.

Ni nani atakayeweza kufikia habari ninazotoa?

Habari zinazochukuliwa kutoka kwa utafiti huu zitahifadhiwa salama kwenye kabati zilizofungwa na kompyuta zinazofunguliwa kwa neno maalum. Habari hizi zitapeanwa tu kwa watu wanaohusika na utafiti kwa ukaribu. Habari zitawekwa kwa muhtasari na majina yote ya washiriki yataondolewa kutoka kwa stakabadhi. Habari za utafiti huu zinaweza kutumika kwa kazi ya baadaye; habari zitatolewa tu baada ya kamati huru ya kitaifa itakapoangalia na kukubali kwamba hutaathirika kwa njia yoyote.

Je nikiwa na maswali yoyote?
Uko huru kujadili uamuzi wako kuhusu kushiriki kwenye utafiti huu na mzazi/mlezi wako au watu wengine na unaweza kuomba kupewa muda uende ujadiliane nao.

Uko huru kuuliza maswali mfanyikazi wetu yeyote wakati wowote. Unaweza kuwasiliana na kundi la utafiti kwa kutumia anuani zifuatazo
Dkt Ifedayo Adetifa, KEMRI Wellcome Trust Research Programme, S.L. Posta 230, Kilifi. Simu: 0721 337 598 au 0722 203417, 0733 522063, 041 7522063

Ikiwa unataka kumuuliza mtu huru chochote kuhusu utafiti huu tafadhali wasiliana na:

Meneja wa kitengo cha uhusiano mwema na jamii, KEMRI Wellcome Trust Research Programme, S. L. Posta 230, Kilifi. Simu: 041 7522 063, Rununu 0723 342 780 au 0705 154 386

Na
Kiongozi, Kitengo cha kukagua sayansi na maadili cha KEMRI S. L. Posta 54840-00200, Nairobi; Nambari za simu: 0717 719477; 0776 399979 Anwani ya barua pepe: seru@kemri.org

Fomu ya ruhusa ya shirika la utafiti la KEMRI Wellcome Trust ya Kuelewa ueneaji, usimamizi na matokeo ya COVID-19 hapa Kenya

Mimi, _____ (jina la mshiriki), nimeelezwa kuhusu utafiti huu. Nimeelewa yote yaliyosomwa/elezewa na maswali yangu yamejibiwa kikamilifu. Ninakubali kushiriki katika utafiti huu.

Ninaelewa kwamba kushiriki kwenye utafiti huu kutahusisha kusafirisha sampuli zangu ng'ambo, ikiwa ni pamoja na Marekani na Thailand

Nakubali sampuli zangu zihifadhiwe kwa matumizi ya utafiti wa siku za usoni. Ndio ☐ La ☐

Nakubali sampuli zangu zisafirishwe ng'ambo kwa matumizi ya utafiti wa siku za usoni. Ndio ☐ La ☐

Ninaelewa kwamba ninaweza kubadilisha mawazo yangu katika hatua yoyote na haitaniathiri kwa njia yoyote

Sahihi ya mshiriki: _____ Tarehe_____

Jina la mshiriki: _____ Saa _____

(Tafadhali andika jina kwa herufi kubwa)

Kama mtoto hawezi kusoma, hakikisha shahidi* anashuhudia uombaji wa idhini na kuweka sahihi hapo chini:

Nathibitisha kwamba habari kuhusu utafiti huu zimeelezewa kwa usahihi na ni wazi kwamba mtoto amezielewa na kwamba mtoto ametoa idhini kwa hiari.

Sahihi ya shahidi _____ Tarehe_____

Jina la shahidi_____Saa _____

(Tafadhali andika jina kwa herufi kubwa)

**Shahidi ni mtu huru kutokana na utafiti au mfanyikazi ambaye hakuhusika na kuomba idhini*

Alama ya dole gumba la mshiriki aliyetajwa hapo juu iwapo hawezi kuandika: _____

Nimefuata utaratibu wa utafiti kuomba idhini kutoka kwa mshiriki. Ni wazi ameelewa hali na lengo la utafiti na ametoa idhini ya kushiriki katika utafiti huu. Amepewa fursa ya kuuliza maswali ambayo yamejibiwa kikamilifu.

Sahihi ya muwakilishi/mtafiti_____ Tarehe_____

Jina la muwakilishi/mtafiti_____ Saa_____

(Tafadhali andika kwa herufi kubwa)

MSHIRIKI SASA NI APEWE NAKALA ILIYOWEKWA SAHIHI AJIWEKEE